UHURU UK 6

## ...ifariki dunia juzi

# Ndaki aeleza mradi wa machinjio unavyotafsiri dhamira ya serikali

**Na LATIFA GANZEL**, *Morogoro*

SERIKALI imesema mradi wa machinjio ya kisasa wa Ranchi ya Nguru Hills, wilayani Mvomero mkoani Morogoro, umetafsiri dhamira ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kupambana na umaskini kutokana na kutoa ajira kwa watanzania.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizindua kiwanda hicho kilichopo wilayani Mvomero.

"Sekta za mifugo na kilimo ni kubwa nchini, watanzania walio wengi wamejiajiri, hivyo inapotokea uwekezaji katika eneo hilo, tafsiri yake ni kwenda kuwainua wafugaji na wakulima ambao ndio kundi kubwa," alisema.

Waziri huyo aliagiza ajira ambazo zinaweza kufanywa na watanzania, wapewe fursa hiyo na si kila kazi kufanywa na wageni.

Alisema mradi huo wa machinjio ya kisasa, utawasaidia wafugaji kupata soko la uhakika wa mifugo yao, wakulima kuuza bidhaa mbalimbali na kunenepesha ng'ombe kabla ya kuchinjwa.

Ndaki alisema pato la serikali, pia litaongezeka kupitia kodi mbalimbali na kuleta fedha za kigeni kutokana na mauzo ya nyama katika soko la nje.

Alieleza wananchi wanaoishi kuzunguka kiwanda hicho, watanufaika na fursa mbalimbali zinazotokana na uwepo wa mradi huo.

Akifafanua zaidi, Ndaki alisema biashara ya nyama katika soko la nje, linaendelea kukua kwa kasi kwani mwaka 2020/2021, Tanzania iliuza tani 1,774 katika masoko mbalimbali ya kimataifa, huku 2021/2022 tani 10,413 ziliuzwa.

Kuanzia Julai hadi mwezi uliopita, Tanzania ilisafirisha tani 4,374 za nyama zenye thamani ya dola za Marekeni 16,760,284, katika masoko ya nje.

Aliwataka wafugaji kubadilika kwa kunenepesha mifugo kutokana na mazingira yanayowekwa na serikali.

Waziri alibainisha mazingira hayo ni kuwepo viwanda ambapo wizara, imeanza mpango wa mabadiliko ya sekta ya mifugo kwa nia ya kuwa na mifugo itakayowezesha kupata malighafi.

**MKURUGENZI MKUU PSSSF**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), CPA Hosea Kashimba, alisema mradi wa machinjio, umegharimu dola za Marekani milioni 15 kwa ununuzi wa mashine na mitambo.

Pia, ukarabati wa jengo la kiwanda, ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka, ujenzi wa barabara ya kuingia kiwandani na gharama za uendeshaji.

Kashimba alisema uwekezaji wa wanahisa wengine ni dola milioni 10, huku dola milioni tano ikiwa ni mkopo kutoka Benki ya Azania. PSSSF imewekeza dola milioni 3.9, kati ya dola milioni 10. Uwekezaji huo, unaifanya PSSF, kuwa na asilimia 39 ya hisa.

Wawekezaji wengine wabia ni Kampuni ya Eclipse Investment LLC ya Oman yenye hisa 46 na Kampuni ya Busara Investment LLP yenye hisa asilimia 15.

Alisema mradi huo unatarajiwa kuleta manufaa mbalimbali kwa jamii ikiwemo ajira za moja kwa moja 350 na zingine za ziada 2,000, zinazotokana na mnyororo wa thamani.

Pia, Kashimba alisema mradi unalenga masoko ya ndani na nje ya nchi, hivyo ni matarajio asilimia 80 ya soko, itakuwa nje ya nchi na asilimia 20 kwa soko la ndani.

**RC MWASA**

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa, alisema wamejiwekea mkakati wa kuanzisha ranchi sita za unenepeshaji ng'ombe kutoka kilogramu 120 hadi kufikia kilogramu 250 kwa mahitaji ya kiwanda cha nyama cha Nguru Hills.



na Ofisi ya Waziri Mkuu).

# Vijana wajivunia kuvuna samaki 3,000

**Na BALTAZAR MASHAKA,** *Ilemela*

VIKUNDI vya vijana vya CHAPAKAZI na CATFISH vinavyojishughulisha na ufugaji wa samaki kwa vizimba vimeanza kunufaika na mradi huo kwa kuvuna 3,000.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Vijana wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Lucy Nicholaus, wakati wa uvunaji samaki awamu ya kwanza ya mradi wa vikundi hivyo.

Vikundi hivyo vilivyokopeshwa na halmashauri hiyo sh. milioni 91.88 za mapato ya ndani, Aprili, mwaka huu.

"Tunashuhudia matunda ya vikundi viwili vya vijana vya CHAPAKAZI na CATFISH wanaojihusisha na uvuvi hapa Igalagala, baada ya miezi sita wakihangaika kwa ufugaji wa samaki kwa vizimba, hatimaye leo (jana) wameanza kuvuna walichokipanda," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kikundi cha CATFISH, Baraka Buhegu, alieleza mradi wao ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020-2025 kutokana na serikali kuimarisha sekta ya uvuvi, kuongeza matumizi ya teknolojia ya uvuvi endelevu katika kupambana na kuepuka uvuvi haramu.

Aliongeza kuwezesha sekta ya uvuvi kuchangia zaidi ukuaji uchumi wa taifa, kuzalisha ajira kwa vijana na kuboresha maisha ya wavuvi na wananchi kwa ujumla.

Baraka aliishukuru Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa kuwaamini na kuwapatia fedha zilizowawezesha kufuga samaki kwa vizimba, ambao ni wa kisasa, hivyo kuwasaidia kujikwamua na umaskini wa kipato.

Aliipongeza serikali kwa kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa zana bora za uvuvi, kuzuia uzalishaji na uagizaji wa zana haramu za uvuvi, kuhamasisha uwekezaji wa kuzalisha vyakula vya samaki, kuwawezesha vijana mitaji na kumudu kujiajiri.

"Leo (jana) tumevuna samaki 3,000 tunaotarajia kuwauza shilingi 5,000 kwa kila mmoja, matarajio yetu kupata shilingi milioni 15 na baadhi ya wateja tunao," alisema Baraka.

Alisisitiza samaki waliowavuna ni wa viwango na wana ubora wenye radha halisi.

Ofisa Uvuvi wa Manispaa ya Ilemela, Ivon Maha, alisema mradi huo ulibuniwa na vijana wenyewe na kuungwa mkono na wataalamu wa uvuvi hadi kuvuna samaki.

Meneja mradi wa uimarishaji wa mabaraza ya watoto kutoka Shirika la Rafiki-SDO, Tangi Clement, akizungumza na viongozi wa Baraza la Watoto katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, kuhusu kupaze sauti zao juu ya vitendo vya ukatili ambavyo wanafanyiwa juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

NIPASHE UK 24.

# Wavuvi 'waiangukia' serikali waongezewe muda

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya wavuvi na wamiliki wa mitumbwi wanaofanya shughuli zao katika Ziwa Victoria, wameiomba serikali kuwaongezea muda ili kuachana na matumizi ya taa za betri kwa ajili ya shughuli za uvuvi wa dagaa.

Wavuvi hao wanatakiwa kutumia taa za mwanga wa jua (solar), badala ya taa zinazotumia betri katika shughuli zao za uvuvi.

Walisema ikiwa wataacha kutumia betri hizo kwa sasa bila kujiandaa watapata hasara kutokana na kutumia fedha nyingi kuzinunua.

Pia agizo hilo limekuja ghafla kutokana na baadhi ya wavuvi kufanya uwekezaji katika taa hizo na kusitisha matumizi yake kunaweza kuwasababishia hasara.

"Tunaomba kuongezewa muda hata kufikia mwezi wa sita mwakani ili na sisi tuweze kujiandaa kwani hata hivyo utafiti wa kubaini madhara yake bado haujafanyika kikamilifu maana hatujaambiwa ukali wa mwanga wa taa tunazozitumia kwa sasa na zile wanazotaka tutumie," alisema Mandondo Maro, mmiliki wa mtumbwi.

Edward Manna, mvuvi wa dagaa akizungumzia hatua hiyo alisema alikuwa amechukua mikopo na kuweweza katika taa hizo.

Alisema alikuwa hajui kama taa hizo ni haramu na kuzisitisha ghafla kutamsababishia aingie kwenye madeni ambayo uwezo wa kulipa ni mdogo.

Akitoa ufafanuzi kuhusu marufuku hiyo, Kaimu Ofisa Mfawidhi ulinzi na usimamizi na rasilimali za wavuvi Kanda ya Ziwa, Laurent Mbujiro, alisema matumizi ya taa hizo ni ukiukwaji wa kifungu namba 16 kifungu kidogo (ii) cha sheria za uvuvi.

Novemba 17, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akiwa mkoani Mwanza, alitoa muda wa miezi miwili kwa wavuvi wanaotumia taa za umeme wa jua zinazotumia betri kuacha kwa kuwa zinadaiwa kuwa kichocheo cha uvuvi haramu na kuharibu mazalia ya samaki katika Ziwa Victoria kutokana na kuwa na mwanga mkali.

Aidha, aliwataka wavuvi wa dagaa kutumia taa zenye mfumo wa umeme jua moja kwa moja badala ya zinazounganishwa na betri kutokana na kubainika kuwa na madhara.

MWANANCHI UK13.





>>Uvuvi endelevu

# Nyavu za timba zinafunga kizazi cha samaki

**Mwandishi Wetu**, Mwananchi
uchumi@mwananchi.co.tz

**Mpwapwa.** Kutokana na athari za kutumia kemikali zinazoathiri mazalia ya samaki, Serikali imekemea uvuvi haramu ili kuzifanya rasilimali hizo kuwa endelevu.

Onyo hilo limetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene alipozungumza na wananchi wa Kata ya Mtera iliyopo katika Jimbo la Kibakwe wilayani Mpwapwa, kusikiliza na kutatua kero zao.

"Msitumie nyavu za timba ambazo zina sumu zinazoua mazalia ya samaki na kusababisha madhara hata kwa mtumiaji wa samaki waliovuliwa kwa nyavu hizo," amesema Simbachawene.

Matumizi ya nyavu hizo amesema yanasababisha bwawa hilo kutokuwa endelevu kwani hakuna uvuvi unaoendelea kutokana na kukosekana kwa samaki.

"Ofisa uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kwa kushirikiana na maofisa uvuvi katika maeneo yanayozunguka Bwawa la Mtera andaeni andiko litakalosaidia kuja na mkakati wa uvuvi endelevu katika Bwawa la Mtera," amesema Waziri Simbachawene.

**01**

**Bwawa la Mtera ndilo pekee mkoani Dodoma. Ni maalumu kwa ajili ya kuzalisha umeme wa gridi ya Taifa.**

Naye Ofisa Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Fransisco Mwanga amesema matumizi ya nyavu haramu aina ya timba ni hatari kwani zinapowagusa samaki huwafanya washindwe kuzaliana.

"Elimu imetolewa kwa wavuvi na wakati mwingine wanapigwa faini lakini bado wanaendelea na uvuvi haramu uliosababisha samaki kutozaliana," amesema Mwanga.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Hussein Mkwizu alisema utoaji wa elimu kuhusu uvuvi haramu ni suala linalopaswa kuwa ajenda ya kudumu kwenye vikao vya maendeleo vya kijiji ili kujenga uelewa wa pamoja kwa wavuvi na wananchi kwa ujumla, kwani wao ni walaji wa samaki wanaopatikana.

"Hakuna kambi inayolizunguka Bwawa la Mtera ambayo haijapitia shida hii, sasa hivi kila mtu anafikiria namna tatizo hili linavyoweza kutatuliwa na lisijirudie," alisema.

Uvuvi haramu unapigwa vita nchini ili kuzifanya rasilimali za majini kuwa endelevu, kwani matumizi ya kemikali au nyavu zenye matundu madogo hupunguza kama si kuondoa kabisa samaki wadogo wanaotakiwa kukua kabla ya kuvuliwa kwa ajili ya kitoweo.



